

RITA- POSTA WAMEKUBALIANA KUSAFIRISHA NYARAKA NA MIZIGO YA WAKALA KATIKA MIKOA YOTE TANZANIA BARA.

Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhamini (RITA) na Shirika la Posta wamesaini hati ya makubaliano ya huduma ya kusafirisha mizigo na nyaraka mbalimbali za Wakala.

Akizungumza hii leo jijini Dar es Salaam katika hafla fupi ya makubaliano hayo Kabidhi wasii Mkuu wa RITA Bi Emmy Hudson amesema kuwa Shirika la Posta limekabidhiwa jukumu la kusafirisha vifaa na nyaraka mbalimbali katika Ofisi za Wakuu wa wilaya, Wakurugenzi na ofisi za watendeji wa Kata na hivyo kuhakikisha usalama na kuwezesha wananchi kupata huduma kwa wakati.

Bi Hudson ameoongeza kuwa Wakala unasafirisha kwa wastani tani 10 za mizigo kwa mwaka ambayo inajumuisha vitendea kazi na nyaraka mbalimbali kama vile fomu za usajili wa vizazi na vifo ambazo zinatakiwa kurudishwa Makao Makuu ili ziweze kutunzwa kwa ajili ya matumizi ya Serikali na watu binafsi.

“Makubaliano haya yatadumu kwa mwaka mmoja na yatasaidia kupata taarifa za vizazi na vifo ndoa na talaka sambamba na vifaa vya kutolea huduma kufika kwa wakati sehemu husika”. alisema Bi Hudson.

Kwa upande wake Mkuu wa Shirika la posta Tanzania Bw Hassani Mwang’ombe amesema kuwa makubaliano hayo yatarahisisha usafirishaji wa mizigo na nyaraka hizo kufika kwa wakati katika Mikoa yote Tanzania Bara na kuwahakikishia wananchi upatikanaji wa huduma bora.

Bw Mwang’ombe ameoongeza kuwa shirika la Posta lina magari na vitendea kazi vya kisasa vyenye uwezo wa kutoa huduma ya usafirishaji wa mizigo, nyaraka na abiria katika Mikoa mbalimbali Tanzania Bara huku shirika likiendelea kufanya maboresho katika mifumo ya teknolojia ya habari na mawasiliano ili mteja anapopatiwa huduma ya usafirishaji aweze kufuatilia kwa kutumia simu ya kiganjani.

“Kwa sasa tumeanza kutumia TEHAMA katika ufuatiliaji na kutunza nyaraka hivyo kuongeza umakini katika utunzaji na Usafirishaji wa mizigo na nyaraka za wateja wetu” alisema Bw Mwang’ombe.

RITA na Shirika la Posta wamekuwa wakishirikiana katika utoaji wa huduma ikiwemo ile ya uhakiki wa vyeti vya kuzaliwa na vifo kwa wanafunzi wanaoomba mkopo wa elimu ya juu ambapo hupatiwa huduma ya mtandao wa kutuma nyaraka zao kupitia vituo maalum katika ofisi za Posta Tanzania Bara.